

Vidokezo vya Usalama Katika Msimu wa Uchaguzi

Uchaguzi wa kitaifa wa rais nchini Marekani hufanyika kila baada ya miaka 4, Jumanne ya kwanza ya Novemba. Wakati huu, watu wanaweza kuangazia zaidi wakimbizi na mashirika ya makazi mapya. Vifuatavyo ni baadhi ya vidokezo na mwongozo wa usalama kwa hali ambazo unaweza kukumbana nazo nchini Marekani. Ikiwa una maswali, zungumza na shirika lako la makazi mapya.

- Ikiwa mtu anataka kukuhoji, una haki ya kukataa. Ikiwa mtu anataka kuchukua video au picha yako, una haki ya kukataa. Unaweza kutumia maneno kama vile “usinipige picha” au “achana nami.” Unaweza pia kufunika uso wako kwa kutumia mkono wako. Usikimbie na usijaribu kupigana na mtu huyu, ila mpuuze na uondoke. Ikiwa unahisi usalama wako uko hatarini, omba usaidizi.
- Mtu akikupigia simu ili kukutishia, usijibu. Andika nambari hiyo ya simu, kile mtu huyo alichosema, ikiwa alikuwa mwanamume au mwanamke, kelele ya mazingira na maelezo mengine yoyote. Kisha kata simu. Zungumza na msimamizi wa kesi yako kuhusu simu hiyo na umwonyeshe madokezo yako. Atakusaidia kuripoti mazungumzo hayo ya simu kwa watekelezaji wa sheria.
- Mtu akikunyanyasa kupitia jumbe za maandishi au mitandao ya kijamii, usijibu. Weka rekodi ya jumbe za maandishi au jumbe za mtandaoni. Zungumza na msimamizi wa kesi yako kuhusu jinsi ya kuripoti jumbe hizo kwa mamlaka husika.
- Usishiriki maelezo ya kibinafsi na mtu yeyote usiyemjua. Mtu akikupigia simu au kukutumia barua pepe kukuomba maelezo kama vile nambari yako ya usalama wa jamii, tarehe ya kuzaliwa, au nambari ya akaunti ya benki, usimpe maelezo haya! Mtu huyu akisema kuwa utafurushwa au kwenda jela usimpompa maelezo hayo, huo ni ulaghai (ujanja)! Ikiwa huna uhakika kuhusu jambo fulani, zungumza na msimamizi wa suala lako kabla ya kuchukua hatua.
- Hakikisha kuwa simu yako, anwani ya barua pepe na akaunti zote za mtandaoni (kama vile akaunti za benki) zina manenosiri thabiti.
- Kuwa mwangalifu na mazingira yako. Usitembee peke yako usiku na ujaribu kutembea mkiwa wawili au katika vikundi. Ikiwa unaona kitu au mtu unayeshuku karibu nawe, mwarifu mwenzako. Ukiwa katika hatari ya dharura, piga simu kwa 911.
- Ukiwa nyumbani, usisahau kufunga milango na madirisha ya nje. Usiwaruhusu watu ambao huwajui kuingia nyumbani kwako. Weka mapazia kwenye madirisha yako na ufunge mapazia usiku. Ikiwa unaendesha gari, hakikisha kuwa umefunga milango na madirisha ya gari.
- Jaribu kubadilisha ratiba na mazoea yako. Ikiwa unapenda kutembea katika mtaa wako, jaribu kwenda kwa nyakati na siku tofauti.

Shukrani kwa Jukwaa la Usalama na Ulinzi wa Makazi Mapya